


# SAWA WANAWAKE TANZANIA (SAWA)

*News letter 01*

01 Utangulizi
02 Dibaji
03 Historia Yetu
04 Maadili ya Shirika
05 Jua zaidi kuhusu Leena pre & primary school
06 Wekeza kwa mtoto
07 Tuwalinde Watoto
08 Access to girls Education-Kasanga Iringa
09 Washirika Wetu

Chapa ya kwanza 2021

Ndani
# YALIYOMO





*Soma*
# UTANGULIZI

Sawa Wanawake Tanzania (SAWA), zamani ilijulikana kama 'Safina Women's Association' ilisajiliwa kama Shirika lisilo la kiserikali mwaka 1998 chini ya Sheria ya Asasi za Kiraia ya mwaka 1954 kanuni Namba. 5 na kupewa usajili Namba. SO.9351. Kufuatia usajili wa lazima wa mashirika yasiyo ya kiserikali, SAWA ilisajiliwa upya na kupewa jina jipya 'SAWA WANAWAKE TANZANIA (SAWA)' na kuthibitishwa kwa usajili Na.00NGO/R/0221.

## Mtazamo wa shirika

SAWA kama shirika lisilo la kiserikali lina mtazamo wake, ambapo limejikita katika kusaidai na kuwainua wanawake,wasichana wadogo na watoto kwa kuangalia mahitaji yao kwa kuhakikisha wanapata haki zao za msingi na kuboresha maisha yao .

## Dira

Shirika limedhamiria kufikia dira yake kupitia hatua mbalimbali kama vile: utetezi,mafunzo na uhamasishaji miongoni mwa watoto, wanawake na wanajamii kwa ushirikiano wa serikali za mitaa na serikali kuu,wanajamii na wadau mbalimbali katika kuboresha malezi na makuzi ya mtoto,elimu ya msingi na sekondari na mifumo ya ulinzi wa mtoto kwa jamii.

Kwa sasa SAWA inafanya kazi katika mikoa ya Iringa wilaya ya Mufindi na Morogoro wilaya ya Mvomero. Kupitia miradi ya 'Tuwalinde Watoto, Wekeza kwa mtoto na mingine,' SAWA imefanya kazi kwa mafanikio katika sekta ya elimu na ulinzi wa mtoto. Ujenzi wa miundo mbinu ya shule na kampeni ya ulinzi wa mtoto ,imesaidia sana kufikisha huduma ya elimu na ustawi wa mtoto katika wilaya ya Mvomero.

## Malengo

Kufikia 2030, watoto wote wapate na kufaidika na nafasi za kujifunza, kuboresha afya zao na kupatiwa ulinzi na usalama wanaostahili

# ENEO TULIPO

Kitabu hiki kimeandaliwa na Sawa Wanawake Tanzania (SAWA), Shirila la SAWA lipo umbali wa kilometa 5.7 ukitokea Kituo kuu ya mabasi Msamvu na ukitokea manispaa ofisi zipo umbali wa Kilometa 3. Shirika la SAWA linapatika Kigurunyembe mkabala na Kola Hill Secondary. Kupitia barabara ya zamani ya Dar es salaam.


**Mwandishi:**

Adam Memba

**Mchapaji na mbunifu:**

Samuel Mwaleni

**Mawasiliano:**

S.L.P 6031, Morogoro, Tanzania.

Simu: +255 713 518949

+255 655 000421

Barua pepe: sawa98@gmail.com

Tovuti: www.sawawanawake.or.tz

Mtandao wa kijamii: SawaWanawakeTZ

Sawa Wanawake Tanzania



*Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili ama kutumia picha kwa sababu zozote za kibiashara. Kitabu hiki kitumike kufikisha taarifa muhimu za shirika la* Sawa Wanawake Tanzania (SAWA). *Ikiwa utahitaji kukitumia kwa matumizi tofauti tafadhali wasiliana na uongozi.*


.

*Soma*

# DIBAJI

Kufikia 2030, tunatarajia watoto wote wapate na kufaidika na nafasi za kujifunza, kuboresha afya zao na kupatiwa ulinzi na usalama wanaostahili. Hivyo kama shirika tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa wafadhili, wadau, na mashirika mengine yaliyoshirikiana nasi na yale tunayoendelea kushirikiana nayo bega kwa bega pamoja na wanajamii ili kufikia lengo la kuhakikisha tunaboresha malezi na makuzi ya mtoto, elimu ya msingi na sekondari pamoja na mifumo ya ulinzi wa mtoto. Rai yetu kwa serikali ni: tunaomba ushirikiano wa hali na mali pale tunapowahitaji.



# Historia ya Shirika

Shirika la SAWA lilianzishwa kama kikundi mwaka 1996 kwa jina la SAFINA WOMEN ASSOCIATION (SAWA). Waanzilishi ni akina mama wajane, wakiwa na lengo la kuinuana kiuchumi kwa kuanzisha VICOBA ili kuweza kuweka akiba na kukopeshana ili kusomesha watoto na kununua viwanja kwa ajili ya makazi kwani wengi wao walikuwa hawana kipato cha kuwatosheleza kukidhi mahitaji ya familia zao. Kikundi hiki cha akina mama kilijiwekea mikakati ya kukutana ili kujadili mipango itakayofanya kikundi kinaendelea kuwa hai na kutimiza malengo waliojiwekea. Pia kuhusu elimu wazazi wengi walisomesha watoto wao katika shule za serikali yaani Msingi na Sekondari kutokana na hali zao kiuchumi na kipindi hicho nyingi kati yazo hazikuwa zikifanya vizuri kitaaluma jambo lililopelekea Wazazi wenye uwezo kifedha kusomesha watoto wao nje ya Mkoa wa Morogoro, hapo ndipo lilipoibuka wazo la kuanzisha shule yenye viwango na kutoa elimu kwa gharama nafuu ili kukomboa watoto wa wazazi wenye vipato vya chini. Ndipo kwa nguvu zao na ufadhili wa Leena na Pertti Seppanen kupitia shirika la STO Finland, kukaanzishwa shule ya Awali na baada ya miaka michache kuunzishwa shule ya Msingi. Kufikia 1998 Shirika la Safina Women`s Association (SAWA) lilipata usajili mpya kwa jina la SAWA WANAWAKE TANZANIA (SAWA) kama shirika lisilo la kiserikali kwa usajili No. 00NGO/R/0221 na kufikia 15/7/1999, Leena Pre and Primary School ilifunguliwa na kuwekwa jiwe la msingi na kuanza kutumika.

*Hellen Nkalang`ango*
*Mkurugenzi*
*Sawa Wanawake Tanzania (SAWA)*



Ili kutimiza majukumu yake Shirika limezingatia maadili yafuatayo:

* Uwazi
* Usawa wa kijinsia
* Ari/Morali ya kufanya kazi kama timu
* Uadilifu
* Ushirikiano na Asasi/mashirika mengine
* Utoaji wa matokeo kwa wakati/ripoti

Karibuni tuwapitishe katika utendaji wa shughuli mbalimbali zinazofanywa na shirika la SAWA WANAWAKE TANZANIA (SAWA).

Miradi iliyotekelezwa na inayotekelezwa na SAWA

1. **Wekeza kwa Mtoto**
2. **Tuwalinde Watoto**
3. **Leena Pre and Primary School**
4. **Access to girls Education**

**<u>Mahali Miradi Inakotekelezwa</u>:**

Mkoa wa Morogoro: Morogoro Manispaa, Wilaya ya Mvomero, na Iringa - Wilaya ya Mufindi.



*Jua zaidiKuhusu*

# WEKEZA KWA MTOTO

## Shule



Mradi huu ulianzishwa na kutekelezwa 2012-2020 kwa ufadhili wa Firelight Found. Ulihusisha ujenzi wa vituo shikizi viwili(satellite schools) kwa jamii za wafugaji katika vitongoji vya Matangani na Vianzi.

Kufikia sasa kuna jumla ya vyumba vya madarasa 8 na chumba 1 cha ofisi, kati ya madarasa hayo 8 darasa 1 ni darasa la awali.

Pia ina jumla ya matundu ya choo 8 kwa ajili ya wanafunzi wa kike na wakiume, na tundu 1 la choo kwa ajili ya walimu.





## Kliniki

Huduma ya kliniki katika kitongoji cha Vianzi. Kwa kushirikiana na wilaya ya Mvomero tunatoa elimu ya afya ya uzazi, uzazi wa mpango, umuhimu wa kinga kwa watoto n.k. tumewafikia watu 4876 tangu 2013.

Huduma hii ya kliniki imesaidia sana kwa mama na mtoto kupata kwa wakati chanjo kwa watoto wao na huduma ya uzazi wa mpango. Pia imesaidia watoto kuwa wenye afya njema, kwakuwa wahudumu wa afya wamekuwa wakiwapa mafunzo ya namna ya kuwanyonyesha pindi tu wanapotoka kujifungua na kuandaa lishe bora ya watoto wao wanapofikisha umri wa kuanza kula ambao ni miezi 6.

*Tumeifikia jamii kubwa na kufanya inufaike na miradi yetu*

*Jua zaidi Kuhusu*

# Leena Pre and Primary School



Sawa Wanawake Tanzania (SAWA) inasimamia shughuli za elimu katika shule hii iliyo ndani ya manispaa ya Morogoro kwa udhamini wa Social Teachers Organization in Finland(STO) tangu mwaka 2000 hadi sasa. Shule hii inatoa elimu jumuishi(inclusive education) bila kubagua watoto wenye ulemavu(viziwi) na wasio na ulemavu.

Shule ya Awali na Msingi Leena ina jumla wanafunzi 276 wa kike 137 na wa kiume 139. Na wenye ulemavu 15 kati yao wa kike 2 na wa kiume 13. Pia, ina Jumla ya walimu 13, wa kiume 9 na wa kike 4.



Wanafunzi wakiwa pamoja wakiimba na kucheza kipindi cha asubuhi kabla ya kuingia darasani. Kwa kawaida shule imekuwa ikiwakutanisha wanafunzi mapema asubuhi kabla kuanza kwa vipindi vya masomo.

Wakati huu ndio watoto upewa mazoezi ya mwili, kuimba, kufanya mijadala mifupi na mwisho matangazo ya siku husika/ jambo litakalofanyika siku zijazo.



Wanafunzi wakiwa darasani pamoja na mwalimu wao, kwa kawaida shule ya Leena kila mtoto anakaa katika dawati lake ili kupunguza msongamano katika darasa, pia inaweka nafasi nzuri kwa mwalimu kumfikia kila mwanafunzi kwa urahisi na kuweza kumsaidia.

Njia hii imesaidia kuongeza ufanisi kwa walimu na wanafunzi kufanya vizuri kwenye masomo.

# Wanafunzi wanasema nini?



Lisamanu A. Mapinduzi

**Lisamanu A. Mapinduzi**, nasoma darasa la 6 katika shule ya awali na msingi Leena, Morogoro. Nikiwa shuleni nafurahia sana masomo yangu, ninawashukuru walimu wangu kwa kuniwekea msingi mzuri kwa ajili ya wakati ujao. Mimi baada ya kumaliza masomo yangu, ninatamani sana kuja kuwa mhandisi wa barabara.

Nawashauri wazazi wengine wawalete watoto wao hapa leena, kuna walimu wazuri wamenisaidia sana.

**Zubeda H. Omary**, nasoma darasa la 5 katika shule ya awali na msingi Leena, Morogoro. Naipenda sana shule yangu ya Leena, walimu hapa ni wazuri ni rahisi kuwafikia ili kukusaidia katika masomo. Ninawapenda sana walimu wangu.

Baada ya kumaliza masomo yangu ninatamani kuwa Mwalimu, ni kazi ninayoipenda sana. Ninapenda walimu wanavyofundisha watoto.

Wazazi nawashauri wawalete watoto wao waje kusoma pamoja nasi hapa leena.



**Zubeda H. Omary**



Simpert E. Mhogoma

**Simpert E. Mhogoma**, nasoma darasa la 6 katika shule ya awali na msingi Leena, Morogoro. Nafurahia sana kuwa leena, shule ni nzuri na walimu hapa wanatufundisha vizuri. Kwa sasa nipo darasa la 6 mwaka 2022 nitakuwa darasa la 7 nina uhakika kuja kufanya vizuri katika mitihani yangu kwa jinsi walimu wanavyotufundisha.

Mimi nitakapokuja kumaliza masomo yangu nina tamani kuwa Mwanajeshi.

Njoo leena mtoto mwenzangu



*Kuhusu Leena*

# Wazazi Wanasemaje?

### MZAZI 1:

***Shule: Unamaoni gani kuhusu shule ya leena?***

**Mzazi:** Ni shule nzuri, ina mazingira mazuri na bora kwa watoto wa rika na hali zote wanaweza kusoma hapa kwakuwa hawabaguliwi wala kuwanyanyapaa, zaidi ya yote walimu hapa wanafundisha vizuri hata wazazi tumeridhika watoto wetu kuwa hapa Leena.

***Shule: Unaweza kuwaeleza nini watu wasioifahamu shule ya Leena?***

**Mzazi:** Napenda kuwaambia wazazi wengine kuwa wawalete watoto wao hapa kwa kuwa ni mahali sahihi kwa watoto wao kupata elimu.

***Shule: Ushauri wako ni nini kwa shule?***

**Mzazi:** Walimu waendelee kufanyakazi zao kwa bidii ili kutuletea matokeo mazuri zaidi. Ikiwezekana siku moja shule ishike namba moja kitaifa.

### MZAZI 2:

***Shule: Unamaoni gani kuhusu shule ya leena?***

**Mzazi:** Shule ni nzuri sana, kilichonivutia hapa ni watoto wote hata wenye ulemavu tunasoma nao darasa moja bila kuwatenga na tuna-waona wakiwa na maendeleo mazuri, tofauti na shule zingine. Gharama zake si kubwa sana ukilinganisha na shule zingine za binafsi hivyo hata wazazi wenye kipato kidogo wanaweza kugharamia masomo.

***Shule: Unaweza kuwaeleza nini watu wasioifahamu shule ya Leena?***

**Mzazi:** Ni shule nzuri kwa ajili ya watoto wao hata kama wanaulemavu hapa wanaweza kupokelewa inafariji sana.

***Shule: Ushauri wako ni nini kwa shule?***

**Mzazi:** Nawashauri wazazi wenzangu wasiogope kuwaleta watoto wao leena, hapa ni mahali salama kwa watoto.



Jua zaidi Kuhusu

# TUWALINDE WATOTO

Mradi huu unafadhiliwa na ChildFund Korea tangu 2018 mpaka sasa. Umejikita katika sekta tatu: Malezi kwa makuzi na maendeleo ya mtoto, elimu msingi na ulinzi kwa mtoto.Unatekelezwa katika jamii 19 zilizo katika vijiji 7 ndani ya wilaya ya mvomero ambavyo ni: Ndama Maasai, Kisanga, Matale Dibamba, Dakawa, Mtipule and Lusanga. Kufikia sasa vituo vya kulelea watoto na shule za awali 6 vimejengwa na shule za msingi 4 zenye madarasa 33 zimejengwa, nyumba za waalimu 11 na matundu 8 ya vyoo.



Baada ujenzi wa madarasa kumekuwa na matokeo chanya, ufaulu wa wanafunzi umeongezeka kutoka 38% hadi 90% mwaka 2020. Mahudhurio ya wanafunzi yameongezeka na kupunguza utoro.

Pia, walimu wa kike wameongezwa katika shule ambazo mwanzo hazikuwa na walimu wa kike. Na hii imekuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi wa kike kuweza kupata ushauri nasaha na namna ya kujitambua na hivyo kuepuka vishawishi katika mazingira yao.

## Vituo vya ECD

Vituo vya makuzi na maendeleo ya mtoto (ECD CENTERS). Hivi ni vituo vinavyojengwa SAWA kwa ushirikiano na jamii. Nguvu kubwa imeelekezwa katika jamii za wafugaji zizilizo katika maeneo yasiyofikika kirahisi hali inayopelekea watoto katika jamii hizo kukosa elimu. Mpaka sasa vituo 7 vyenye madarasa yasiyopungua 3 vimejengwa na 4 kati ya hivyo vimetambuliwa na serikali kama shule shikizi na kupatiwa waalimu.





## VICOBA(Village Community Bank)

Shirika la SAWA hutoa elimu ya ujasiriamali, kutunza fedha na jinsi ya kukuza mitaji, ikiwemo kuwapa mikopo ya fedha vikundi vidogo vywenye idadi ya watu kati ya 25 hadi 30. Na kuna jumla ya vikundi 22 tunavyovisimamia.

Na mikopo hii imewawezesha kukuza biashara zao, kuongeza kipato katika kaya zao na kulipia karo ya shule na hivyo kupunguza umaskini wa kaya.

## VVC ( Washauri wa Kujitolea)



Makuzi na maendeleo ya mtoto. Mradi huu unatekelezwa na SAWA kuanzia ngazi ya familia na jamii kwa ujumla kwa kutumia washauri wa kujitolea (***Village Volunteers Councilors*** **(VVC)** 46 waliopatiwa mafunzo maalum juu ya vichangamshi, afya bora,lishe na ulinzi kwa mtoto kuanzia mwaka 0 - 5. Kufikia sasa tumewafikia watoto 4330. Washauri hawa wanatoka katika vijiji husika vinavyofanyiwa mradi wa Tuwalinde Watoto. Kwa ujumla mradi huu unatekelezwa katika wilaya ya Mvomero, Morogoro.

## Walimu wasaidizi



SAWA hutoa mafunzo ya muda mfupi kwa waalimu walio katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa. Mafunzo haya huzingatia kupata waalimu wazawa wa eneo husika ili kuepuka mgongano wa tamaduni hasa lugha itumikayo katika mawasiliano/kufundishia. Mafunzo hayo huwajengea uwezo wa namna ya kuwalea watoto wanaokuja katika vituo. Pia huzingatia mtaala wa elimu ya awali unaotumiwa na serikali.




Kuna jumla ya walimu wasaidizi 19 walipewa mafunzo, na wote wako katika vituo hivyo kwa ajili ya kuwasaidia watoto. Kati ya Walimu hao 19, walimu 10 walipata mafunzo kwenye mradi wa awamu ya kwanza ya Tuwalinde Watoto, na wengine 9 kwenye mradi wa awamu ya pili ya Tuwalinde Watoto katika Wilaya ya Mvomero.

Miradi yote hii inatekelezwa kwa ufadhili wa Shirika la ChildFund Korea kwa shirikiana na Shirika la Sawa Wanawake Tanzania (SAWA).

*Mtoto Kwanza*



**MAGDALENA M. LIMBASI**
Mwanafunzi kidato cha Pili

## Mwanafunzi - Shule ya Sekondari Doma

***SAWA: Unamaoni gani kuhusu Bweni na Maendeleo yako ya masomo baada ya kupata nafasi ya kukaa kwenye Bweni?***

**Mwanafunzi:** Ni mwanafunzi wa kidato cha Pili na nina umri wa miaka 15. Kabla ya kuwepo kwa Bweni kwenye shule yetu, nilikuwa nikitembea umbali mrefu kwa ajili ya kuhudhuria shule. Hata hivyo baada ya muda mzazi wangu alinitafutia chumba ili niweze kufika shule kwa urahisi, lakini kulitokeza changamoto nyingine, sasa ilinilazimu nitumie muda zaidi kujipikia chakula, kutafuta maji, kufua nguo zangu, na kukosa muda wa kushiriki mijadala ya masomo na wanafunzi wenzangu.

Nina shukuru baada ya ujenzi wa bweni, nilipata nafasi ya kukaa kwenye bweni. Kweli maendeleo yangu ya masomo yamekuwa mazuri tofauti na mwanzo nilipokuwa nakaa pekee yangu kwenye chumba cha kupanga ambako ilikuwa ni hatari kwangu . Sasa nina muda wa kutosha kujisomea na hata kusoma pamoja na wenzangu, Napata nafasi nzuri kuomba ushauri wa masomo kwa walimu wangu, na hata wanafunzi wenzangu wenye uwezo zaidi ya wangu.



**Mwl. Omary**
Mwl. Mkuu Msaidzi/Mlezi

## Mlezi wa wanafunzi - Shule ya Sekondari Doma

***SAWA: Unamaoni gani kuhusu Bweni na Maendeleo ya wanafunzi katika shule hasa kwa wanafunzi wa kike?***

**Mlezi:** Mradi wa ujenzi wa bweni umekuwa na matokeo mazuri. Nakumbuka kabla ya ujenzi wa bweni na kisima cha maji, watoto walikuwa wakichelewa kufika shuleni kwa wakati na bado wanapofika walipaswa kwenda mbali kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wote na walimu. Kwa sababu ya umbali watoto wa kike walishawishiwa na vijana wa kiume kwa kuwadanganya kwamba watapa masaada wa kubeba maji kutoka mtoni mpaka shuleni na baadae kuwataka kimapenzi jambo lililopelekea wasichana wengi kupata mimba za utotoni.

Tunashukuru sana shirika la SAWA pamoja na washirika wao ChildFund Korea kwa ujenzi wa Bweni na Kisima kirefu cha maji, tatizo la mimba limepungua kwa asilia 90, mahudhurio darasani yameongezeka, na matokeo yamekuwa mazuri kwa wanafunzi kwasababu yanapata muda mwingi wa kujisomea.

## SHULE YA SEKONDARI KASANGA



Ni shule ya sekondari katika mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufindi. Kitambulisho cha shule ya necta ni S3147. Shule hiyo ni ya wanafunzi wa kiwango cha kawaida tu ambayo ni fomu I - IV. Ilianza tangu 2007 ambapo  mahafali ya kwanza yalikuwa 2010. Shule hiyo ina jumla ya madarasa 14, maabara tatu za sayansi '. Shule inakabiliwa na changamoto tofauti kama; kutokuwepo kwa vyombo vya maabara katika maabara zote.

Shirika la SAWA kwa kushirikina na Shirika la Cotswold ilikuja na mradi wa kuweza kuinua elimu ya mtoto wa kike katika shule ya sekondari Kasanga iliyopo katika mkoa wa Iringa baada ya kuona hali ambazo mtoto wa kike anakabili na kufanya washindwe kufikia ndoto zao za masomo na kisha kuweza kujitegeme na kujenga taifa.

Ukiondoa changamoto ya ukosefu wa vifaa katika maabara, changamoto nyingine ilikuwa ukosefu wa bweni kwa ajili ya wasichana. Wasichana wanatembea mwendo mrefu kufika shuleni, wakipita maeneo yasio salama kwao na hivyo kupelekea kupata vishawishi vya lifti kutoka kwa waendesha bodaboda  hivyo kupelekea kupata mimba za utotoni na kuharibu mustakabari wa masomo yao.



Ili kumuokoa mtoto wa kike katika hatari, hivyo Shirika la SAWA lilitafuta ufadhili kutoka Shirika la Cotswold ili kujenga bweni zuri na la kisasa kwa ajili ya kupunguza umbali mrefu wanaotembea, kwa hakika mradi huu umeweza kupunguza mimba za utotoni kwa wanafunzi wa kike na kuongeza ufaulu katika masomo yao. Wanafunzi wamekuwa na wakati wa kutosha kujisomea masomo yao wawapo kwenye bweni, zaidi ya kuhakikisha masomo yao wanafanya vizuri, bado wasichana hawa wanapata mafunzo ya ujasiriamali kupitia kilimo cha mboga mboga na maua.

Wasichana wote wanaoishi katika bweni wanapata elimu ya ushauri nasaha ili kujiepusha na tabia hatarishi na kuepuka kujiunga makundi yanayoweza kupelekea wao kujiingiza katika mwenendo mbaya.



# Kutoka kwa wadau



**Mwl. Augustino Nyanguli**
Mkuu Msaidizi - Matale

## Mwl. Mkuu Msaidizi

***SAWA: Unamaoni gani kuhusu mradi wa tuwalinde watoto na umeona mabadiliko gani baada ya mradi ukilinganisha na kabla ya mradi?***

Mimi ni Mwl. Mkuu Msaidizi, kabla ya mradi tulikutwa katika hali mbaya sana katika shule yetu. Tulikuwa na miundo mbinu mibovu ya madarasa na vyoo, hatukuwa na nyumba nzuri za walimu, na tulikuwa na upungufu wa walimu. Kukokesana kwa miundo mbinu hiyo kulipekea watoto wengine kusomea nje, kwakuwa tulikuwa na vyumba 5 tu vya darasa.

Nashukuru sana shirika la Sawa Wanawake Tanzania kuja kutujengea miundo mbinu mizuri, ikiwamo vyumba vya madarasa 6, Vyoo matundu 12, Nyumba 2 za walimu zinazobeba familia 4. Haya ni mafanikio makubwa yaliolewa na ChildFund Korea chini ya usimamizi wa shirika la SAWA hapa shule ya msingi Matale. Kumekuwa na ongezeko kubwa la uandikishaji kutoka 50% hadi 90% mwaka 2021. Pia, ufaulu umepanda kwa wastani wa 86% kutoka wastani wa kati ya 20% na 40%.
Tunaishukuru sana CFK na SAWA kwa miundo mbinu hii.



Afisa Elimu Taaluma (**W**) Mvomero

## Mh. Shemahonge

Kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza sana shirika la CFK SAWA kwa kuibua mradi huu mkubwa katika wilaya yetu ya Mvomero. Wangeweza kuupeleka sehemu nyingine, lakini wakaona uhitaji mkubwa katika eneo letu. Tumefurahia uwepo wao pamoja na washirika wao ChildFund Korea kwa kuwa tayari kuwaamini na kuwapa fedha za kutekeleza mradi huu shirika la SAWA.

Serikali itaendelea kuwaunga mkono shirika la SAWA na wadau wengine watakao jitokeza kuja kushirikina nasi. Na tunamani SAWA muendelee kufanyakazi nasi, kututafutia na wadau wengine wa maendeleo kuja kuwekeza katika maendelo ya mtoto. Wilaya yetu ni kubwa sana na ina changamoto nyingi na zinahitaji wadau wa aina yetu.

Tunawashukuru kwa kutupatia vyumba vya madarasa 28, Visima vya maji 10, Bweni katika shule ya Sekondari Doma na Mvomero, lakini na elimu kwa watu wetu.

Huu mradi umetupa hamasa kubwa kwa serikali kuona ni jinsi gani tunatia nguvu na kufanyia kazi maeno yenye changamoto kama vile kupata walimu watakaofundisha katika shule shikizi lakini pia kuona shule hizi shikizi zinakuja kuwa shule rasmi zenye usajili kamili.

# MUUNDO WA SHIRIKA



# WASHIRIKA WETU

ChildFund Korea

Bernard van Leer Foundation

Tanzania Education Network
TenMeT
Mtandao wa Elimu Tanzania
Education: access · equity · quality

Twaweza ni sisi

hakielimu

RELI
Regional Education Learning Initiative

care®

firelight™

kepa

uwezo

Strømme Foundation

CotsWold Family

ILO SCHOOL FINLAND

JOASUE UNIVERSITY

PAULE DOLAN

S.L.P 6031, Morogoro, Tanzania.

Simu: +255 713 518949 au +255 655 000421

Barua pepe: sawa98@gmail.com

Tovuti: www.sawawanawake.or.tz
**tweeter** @sawawanawakeTz , **Youtube:** Sawa Wanawake Tanzanzania,
**Facebook:** @SawaWanawakeTz , **Instagram:** Sawa_Wanawake_Tanzania